

Ilikuwa siku yenye joto jingi.



Siafu Mdogo hakuwa amepata maji kwa siku nyingi.



Akawaza, “Ninahitaji tone moja tu la maji, hata kama litatoka kwenye jani.”



Umande wote ulikuwa umekauka. Hangepata hata tone moja la moja.



Siafu Mdogo akalia sana, “Nisipokunywa maji, nitakufa.Lazima niufikie mto nilioelezwa.”



“Ati mtoni? Huko utakufa maji!” Kichakuro mmoja mwenye hekima alimwonya.



Lakini, Siafu Mdogo hakujali. Kiu chake kiliongezeka. “Nitakufa iwapo sitakunywa maji sasa.” Siafu Mdogo alienda kuutafuta mto alioambiwa juu yake.


N



Alipitia kwenye nyasi
na matawi
yaliyokauka.



Mara akasikia mngurumo wa mawimbi.



Siafu Mdogo alifika mtoni akayanywa maji baridi.



Alifurahi kukata kiu na
hakuliona wimbi
kubwa likija.



Siafu Mdogo alijaribu kujishikilia kwenye nyasi kavu zilizokuwa zikielea. Lakini, alisombwa na maji.



Siafu Mdogo alilia,
“Jamani, nisaidieni.”



Njiwa Mweupe alikuja akamnyooshea tawi. Akasema, “Panda juu ya tawi haraka.” Siafu Mdogo aliruka juu ya tawi na Njiwa Mweupe akamwokoa.





Siafu Mdogo akasema, “Siondoki kabla sijamshukuru Njiwa. Nitasubiri hadi atakaporejea kunywa maji.”



Siku moja alipokuwa akimsubiri Njiwa Mweupe, Jona na Petro walikuja mtoni. Walikuwa wamebeba manati.



“Yule Njiwa Mweupe ambaye huja hapa kunywa maji, tutamla jioni.” Jona akawaza. Jona na Petro walijificha nyuma ya mimea kando ya mto.





“Sitakubali wajanja hao wamuue yule Njiwa Mweupe. Lakini nitafanyaje? Mimi ni mdogo sana.” Siafu aliwaza.



Wakati huo huo Njiwa Mweupe aliruka kutoka mtini anywe maji. Jona na Petro walipima shabaha na kungoja kwa hamu.





Siafu Mdogo alipata wazo.



Aliurukia mguu wa
Petro na kumuuma.



Siafu Mdogo alipata wazo.



Njiwa Mweupe
alishtuka akaondoka.



Hivyo ndivyo Siafu Mdogo alivyomwokoa Njiwa Mweupe.

PRATHAM BOOKS
storyweaver

This book was made possible by Pratham Books' StoryWeaver platform. Content under Creative Commons licenses can be downloaded, translated and can even be used to create new stories - provided you give appropriate credit, and indicate if changes were made. To know more about this, and the full terms of use and attribution, please visit the following link.

Images Attributions:

Page 11: The sight of water, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 12: Water is life, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 13: The wave and the ant, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 14: Ant in water, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 15: Ant swimming in lake, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 16: Dove saves ant, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 17: Drenched ant, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 18: Happy ant, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 19: Boys with dangs, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 20: Boy thinking of meat, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 21: From behind the bush, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license. Page 22: Shocked ant, by Wiehan de Jager © African Storybook Initiative, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license.

Disclaimer: https://www.storyweaver.org.in/terms_and_conditions

Some rights reserved. This book is CC-BY-4.0 licensed. You can copy, modify, distribute and perform the work, even for commercial purposes, all without asking permission. For full terms of use and attribution, http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/